# USAFIRI ARDHINI

Toleo la 2: Oktoba - Disemba 2022




# MHE. MWAKIBETE AIPONGEZA LATRA

- Awataka wananchi waishio maeneo inapopita treni, kuchukua tahadhari ili kulinda maisha na mali zao
- Mkurugenzi wa LATRA awahimiza kuilinda miundombinu ya reli

UK1

## BANTU: CHUKUENI TAHADHARI MNAPOPITA KWENYE MIUNDOMBINU YA RELI

"SGR itakapoanza hapa, treni zitakuwa zinaenda kwa mwendo kasi hivyo tusipozingatia suala la usalama tunaweza kupoteza maisha, kwahiyo usalama katika reli si jambo la kupuuza"...... UK 7

## MADEREVA WATAKIWA KUFUATA SHERIA, KUTOBUGHUDHI ABIRIA



"sisi hatutakuwa na muhali na mtu yeyote na atakayekiuka Sheria atakumbana na mkono wa Sheria, kwahiyo nawasihi kuwa kila mdau atimize wajibu wake."...... UK8

## MADEREVA MBEYA NA RUKWA WAPEWA ELIMU YA UTHIBITISHAJI WA MADEREVA



"Kutokana na elimu tuliyopewa nimegundua kuwa dereva akishathibitishwa anakuwa ametambulika rasmi na anaweza kufanya kazi popote ndani na nje ya nchi. Hivyo ninawashauri madereva wengine tuungane kwa pamoja ili tudhibitishwe"....... UK12



LATRA



# TAHARIRI

**Ndugu Msomaji.**

Karibu katika toleo la pili la Jarida la USAFIRI ARDHINI kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ambalo linaandaliwa na kusambazwa mara nne kwa mwaka.

Jarida hili limekusanya taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ambazo zimefanyika katika robo ya pili ya mwaka yaani kuanzia mwezi Oktoba mpaka Desemba mwaka 2022. Lengo la jarida hili ni kukuhabarisha wewe mdau wetu kuhusiana na mambo ya msingi ambayo Mamlaka inayatekeleza ikiwa ni sehemu ya utoaji wa elimu kuhusu shughuli za Mamlaka na masuala mengine mengi yanayogusa sekta ya usafiri ardhini nchini.

Katika kipindi cha mwisho wa mwaka, LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani tumefanikiwa kwa kiasi kukubwa kudhibiti ajali ambazo kwa miaka ya nyuma zilikuwa zikitusumbua, kupunguza adha ya usafiri kwa kutoa vibali vya muda mfupi kwa magari yaliyokidhi vigezo. Mafanikio haya yamechagizwa na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu usalama barabarani pamoja na ukaguzi maalumu uliofanyika kipindi chote cha mwisho wa mwaka zoezi ambalo tulifanikisha kupitia wataalamu wetu kutoka LATRA na Jeshi la Polisi. Hakika ushirikiano uliopo kati ya taasisi hiz mbili ndio ulioleta matunda mazuri yaliyotupunguzia malalamiko kutoka kwa wadau wa usafiri ardhini.

Mamlaka imeendelea kutoa elimu ya matumizi ya Tiketi Mtandao nchini ili kuhakikisha kwamba wasafiri na wadau kwa jumla wanafahamu kwa kina kuhusu namna ya kukata tiketi kielektroniki mahala popote na kwa wakati wowote ili kuepukana na kadhia zilizopo katika stendi za mabasi.



Mathalani, Desemba 7, 2022, Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Mheshimiwa Nurdin Babu ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Mheshimiwa Kanali Hamis Maiga, alishiriki katika ukaguzi na utoaji wa elimu ya tiketi mtandao katika stendi ya mabasi Moshi.

Pamoja na hayo, tumeshiriki kwenye maadhimisho ya Siku ya Fimbo Nyeupe Duniani yaliyofanyika Kitaifa mjini Babati mkoani Mkoa wa Manyara Oktoba 19 hadi 21, 2022 yenye kaulimbiu 'Ujumuishwaji wa Watu wasioona katika Ajira, Michezo na TEHAMA kwa Maendeleo Endelevu'. Aidha, tumeshiriki katika Mkutano wa 15 wa Mwaka wa Wadau wa Sekta ya Uchukuzi wenye lengo la kufanya tathmini kuhusu maendeleo ya sekta ambapo Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Profesa Makame Mnyaa Mbarawa alisisitiza sekta binafsi kushiriki ujenzi wa miundombinu ili kuharakisha maendeleo na kukuza uchumi wa taifa na mtu mmoja mmoja.

Vilevile LATRA kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Birmingham cha nchini Uingereza tuliandaa mafunzo ya siku tano kwa wataalamu zaidi ya 40 wa usafiri wa reli kutoka nchi 15 za Afrika yaliyofanyika Chuo cha Utumishi wa Umma - Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao jijini Dar es Salaam na tulijadili namna ya kuachana na nishati hatarishi kwa mazingira.

Hayo ni baadhi tu kati ya mengi ambayo utayasoma kwa kina kwenye Jarida hili la USAFIRI ARDHINI. Nami nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kufahamu vizuri maendeleo ya sekta ya usafiri ardhini na udhibiti wa huduma za usafiri ardhini nchini.

Nakutakia usomaji mwema...

**CPA Habibu J. S. Suluo**

# MHE. MWAKIBETE AIPONGEZA LATRA

Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (MB) ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kuendelea kudhibiti sekta ya usafiri wa reli na kuhakikisha kuna usalama kwenye sekta hiyo.

Mhe. Mwakibete amesema hayo Oktoba 13, 2022 alipokuwa akifunga maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli mwaka 2022 kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (MB).

Aidha, Mhe. Mwakibete amesema kuwa LATRA imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya reli katika kutekeleza Sheria ya Reli na kanuni zake kwa lengo la kuimarisha usalama.

Mhe. Mwakibete amewataka wananchi wote wanaoishi maeneo yanayopita treni, kuchukua tahadhari ili kulinda maisha na mali zao "dhamira ya kaulimbiu ya maadhimisho haya inatutaka tuongeze umakini tuwapo katika maeneo ya njia za reli, hivyo niwaombe wananchi tuwe makini kuhakikisha kuwa shughuli za kijamii na kiuchumi hazifanyiki karibu ya miundombinu ya reli."

Akizungumzia majukumu ya LATRA katika uendeshaji wa reli. Mkurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo amesema kuwa LATRA ni msimamizi mkuu wa



*Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (MB) (kulia) akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Sulo*

usalama usafiri wa reli kwa kuhakikisha Sheria na taratibu za uendeshaji wa reli unazingatiwa, pia inatoa ithibati kwa miundombinu mipya iliyojengwa ambapo kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa reli ya kisasa SGR. LATRA itafanya uthibitishaji wa mradi mzima ili uweze kutumika kwa usalama.


Vilevile amesema, majaribio ya uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR unatarajiwa kuanza hivi karibuni, hivyo amewakumbusha wananchi kuchukua tahadhali kwa kutokufanya shughuli katika maeneo hayo, "treni za SGR zina mwendo kasi sana yaani km160 kwa saa, hivyo ni vema wananchi kuwa mbali na reli ili kuepusha madhara."

Vilevile CPA Suluo amewahimiza wananchi kuilinda miundombinu ya reli ili isihujumiwe na watu wachache wenye nia mbaya ya kuharibu uchumi ikizingatiwa kuwa, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya reli na hivyo ni vema tukailinda kwa ajili ya kulinda uchumi wa nchi.

Wiki ya usalama Usafiri wa Reli ilianzishwa na wanachama wa SADC ili kutoa fursa kwa wananchi kufahamishwa matumizi sahihi ya reli katika usafirishaji wa abiria na mizigo. Wiki hii inaadhimishwa katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR. Hivyo kuwezesha usafirishaji kwa njia ya reli kuwa wa haraka na usalama zaidi. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni **Jihadhari, treni zina mwendo kasi na haziwezi kusimama ghafla.**



# PROF. MBARAWA : SEKTA BINAFSI SHIRIKINI UJENZI WA MIUNDOMBINU



Mchoro na dreamstime.com

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amezungumzia umuhimu wa sekta binafsi kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa miundombinu ili kuharakisha maendeleo na kukuza uchumi wa taifa na mtu mmoja mmoja.

Akifungua mkutano wa 15 wa mwaka wa wadau wa sekta ya uchukuzi wenye lengo la kufanya tathmini kuhusu maendeleo ya sekta hiyo nchini, Prof. Mbarawa amesema ushiriki wa sekta binafsi, Serikali na wadau wa maendeleo utaharakisha ujenzi wa reli, barabara, viwanja vya ndege na meli na hivyo kutoa fursa nyingi za ajira na kuhuisha miundombinu ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa.

"Serikali tumejipanga kushirikiana na sekta binafsi katika ujenzi wa barabara mpya ya Kibaha-Chalinze-Morogoro kilomita 215 (express way), ambapo mkandarasi atajenga kwa fedha yake na watakaotumia barabara hiyo watalipia," amesema Prof. Mbarawa.

Amebainisha kuwa Serikali inajipanga kubadilisha Sheria ya TAZARA na TRC ili kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika huduma ya usafiri wa reli kwa kununua mabehewa na kuyaendesha.

Amezungumzia umuhimu wa Tanzania kuwa na miundombinu bora kwa haraka ili kumudu kuhudumia kikamilifu soko la ndani na nchi sita ambazo hutegemea huduma ya uchukuzi kutoka Tanzania, ambazo ni Malawi, Zambia, Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).


Kwa upande wake Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Eng. Kingdom Mbangula akizungumzia ujenzi wa barabara mpya ya kulipia, amesema barabara hiyo itakuwa na njia nne, mbili kwenda Morogoro na Mbili kurudi Kibaha na magari hayatapishana ili kuepusha msongamano na ajali.

" TANROADS tumejipanga ipasavyo kuhakikisha mradi huu unajengwa kwa ubora uliokusudiwa na kukamilika kwa wakati," amefafanua Eng. Mbangula.

Naye Dkt. Patricia Laverley, Meneja Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ameishukuru Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kuandaa mkutano huo wa tathmini wa kila mwaka ambao unaibua changamoto na kuzipatia ufumbuzi kwa haraka.

Amesisitiza kuwa AfDB imetenga asilimia 60 ya bajeti yake katika uwezeshaji ujenzi wa miundombinu ili kuchochea maendeleo ya uchumi kwa nchi za Afrika.

Katibu Mkuu sekta ya Uchukuzi Bw. Gabriel Migire amesema mkutano huo pamoja na mambo mengine utaibua hoja mbalimbali zinazolenga kuboresha sekta ya uchukuzi nchini hivyo kuvutia wawekezaji wengi kupitisha mizigo yao Tanzania na hivyo kukuza uchumi wa taifa.



Mchoro na fatcon.com



# LATRA YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA FIMBO NYEUPE DUNIANI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini imeshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Fimbo Nyeupe Duniani yaliyofanyika Kitaifa mjini Babati mkoani Manyara kuanzia tarehe 19 hadi 21 Oktoba, 2022 yenye kaulimbiu 'Ujumuishwaji wa Watu wasioona katika Ajira, Michezo na TEHAMA kwa Maendeleo Endelevu'.

Mgeni Rasmi katika kilele cha maadhimisho hayo alikuwa Mhe. Patrobas Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa niaba ya Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho hayo, Mhe. Katambi alisema, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maagizo yake amefanya mambo mengi yanayoitekeleza kaulimbiu ya maadhimisho hayo ikiwa ni pamoja na utoaji wa ajira, ujumuishwaji katika maswala ya TEHAMA, uboreshaji wa elimu, uweshaji kupitia mikopo na upatikanaji wa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu.




*Mgeni rasmi wa Siku ya Fimbo Nyeupe Duniani Mhe. Patrobas Katambi (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)( wapili kulia) akiwa na Mkuu wa mkoa wa Manyara Mhe. Makongoro Nyerere wakifuatilia Maadhimisho ya Siku ya Fimbo Nyeupe Duniani yaliyofanyika kitaifa Mkoani Manyara.*

"Serikali ya awamu ya sita imeendelea kujipambanua kwa kuitekeleza Sheria namba 9 ya mwaka 2010 na Sera ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004, ambapo mwaka huu 2022, kati ya ajira 9,800 zilizotolewa Serikalini, viliwekwa viwango vya chini maalum kwa watu wenye ulemavu, hivyo kuwezesha watu wenye ulemavu 261 kuajiriwa, kati yao 61 ni wasioona," alisema.

Aliongeza kuwa, mwaka huu, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa agizo la ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu katika masuala ya TEHAMA na Serikali imeendelea kuwatambua, kuwasikiliza na Kutatua changamoto zao katika nyanja mbalimbali.

"Serikaili inatambua umuhimu na inathamini watu wenye ulemavu, kwa sababu tunajua, hujafa hujaumbika. Serikali imepunguza kodi kwa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu. Kulikuwa na vyuo 7 ambavyo vilikuwa havifanyi kazi, Serikali imevifufua vyuo hivyo ikiwemo chuo cha Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu cha Masiwani kilichopo mkoani Tanga," alifafanua.

Aidha, Mhe. Katambi alisisitiza kuwa kwa mujibu wa Sheria namba 9 ya mwaka 2010, taasisi yoyote inayoajiri watu zaidi ya 20, asilimia 3 wanatakiwa waajiriwe watu wenye ulemavu.

"Tutakagua hadi kwenye viwanda, kama huna watu wenye ulemavu basi ujue unavunja Sheria. Nawaagiza maafisa kazi, ukaguzi ufanyike maeneo yote yanayotoa ajira muhakikishe Sheria hii inazingatiwa. Pia napenda kuwajulisha kuwa Mheshimiwa

***Inaendelea uk wa 4***

# LATRA YASHIRIKI MAADHIMISHO YA...

*Inatoka uk wa 3*



Picha na Pattayathailand.ru

Rais ametoa fedha kuwezesha utengenezaji wa mafuta ya ngozi kwa ajili ya watu wenye ulemavu unaofanyika hospitali ya KCMC na hatuna upungufu."

Pia Mhe. Katambi ametoa wito kwa Mamlaka mbalimbali kuwezesha fimbo nyeupe iwe sehemu ya utaratibu wa alama za barabarani na Sheria itoe adhabu kali kwa wataovunja utaratibu huo.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mhe. Charles Makongoro Nyerere, Mkuu wa Mkoa wa Manyara amewashukuru wafadhili waliowezesha maadhimisho hayo ambao ni pamoja na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, ambapo maadhimisho hayo yamewezesha wadau kujifunza masuala mbalimbali ikiwemo changamoto wanazokabiliana nazo watu wasioona na namna ya kuzitatua.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu J. Suluo alisema kuwa Mamlaka hiyo inatambua na kujali jamii ya watu wenye mahitaji maalum, pia kwa mujibu wa Sheria ya LATRA, kifungu cha 6 (e), Mamlaka ina wajibu wa Kuimarisha Ustawi wa Jamii ya Kitanzania kwa Kuboresha upatikanaji wa huduma za Usafiri Ardhini kwa watumiaji wote ikiwemo wenye kipato cha chini, watu wa vijijini na watu wenye mahitaji maalum. Hivyo, LATRA inaposhirikiana na wadau wa fimbo nyeupe, inatekeleza jukumu la Kisheria.

"Tunaendelea kufanya juhudi mbalimbali ili mtu asiyeona apate haki zake na ajue wajibu wake anapotumia huduma za usafiri ardhini." Alisema

Alifafanua kuwa, mwaka 2019, Mamlaka ilichapisha nakala 130 za toleo la nukta nundu (braille) la Kanuni za Leseni za Usafirishaji kwa Magari ya Abiria na kuzigawa kwa watu wasioona kupitia Chama cha Wasioona Nchini ikiwa ni sehemu ya kuwaelimisha watu wenye ulemavu ili nao washiriki katika maboresho ya kanuni za leseni za usafirishaji kwa magari ya abiria wakati wa kuandaa kanuni hizo.

"Kwa kuwa LATRA iliwashirikisha walemavu, Kanuni za Leseni za Usafirishaji kwa Magari ya Abiria, zilizochapishwa mwaka 2020, zinahusisha haki za walemavu, kwa mfano kanuni hizo zinamruhusu mlemavu kusafiri na kiti chake maalum bila kulipia gharama za ziada." Alisisitiza

Aidha, CPA Suluo alisema, LATRA imekuwa ikishirikiana na Taasisi ya Wasioona (TLB) katika kutoa elimu mbalimbali ikiwemo elimu ya ukataji tiketi kwa njia ya mtandao ambapo kwa sasa, Mamlaka inachapisha nakala 50 katika maandishi ya nukta nundu za Muongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma wenye Ulemavu uliotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora unaoainisha haki na wajibu wa watumishi wa Umma wenye ulemavu na haki na wajibu wa waajiri ili kujenga mazingira wezeshi..

"Jana katika Semina yetu

*Inaendelea uk wa 5*



# LATRA YASHIRIKI MAADHIMISHO YA...

*Inatoka uk wa 4*


hapa mmefundishwa na mtu asiyeona wa hapahapa Manyara, jinsi ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao na tuligawa makabrasha yaliyoandikwa katika mfumo wa nukta nundu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLB) Bw. Omari Mpondelwa alisema kuwa uimara wa chama hicho unategemea aimara wa wanachama, uimara wa Serikali na wadau wengine wa maendeleo katika kutatua changamoto za watu wasioona ambazo ni nyingi.

"Zipo changamoto za unyanyapaa na zingine za watu kutokujua kwa kufanya huruma iliyopindukia. Nawahimiza wanachama kuendeleza umoja na mshikamano utakaotoa taswira nzuri kwa wadau mbalimbali kushirikiana na wasioona kuleta maendeleo," alisema.




# MBEYA NA RUKWA WAPATIWA ELIMU YA TIKETI MTANDAO




*Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Mbeya, Bw. Omary Saleh akikagua Tiketi Mtandao kwa moja ya abiria waliopowa elimu ya Tiketi Mtandao katika Stendi Kuu ya mabasi Mbeya.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani imeendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya Mfumo wa Tiketi Mtandao kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Mbeya.

Elimu hiyo imetolewa na Afisa Mfawidhi Rukwa Bw. Athumani Nyiga, Afisa Mfawidhi Mbeya Bw. Omary Saleh pamoja na Mrakibu wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Rukwa SP Wenceslaus Gumha ambapo kwa nyakati tofauti wamewasihi wananchi na wasafiri wa mikoa hiyo kuendelea kukata tiketi kwa njia ya mtandao kwa kuwa mfumo huo ni rahisi na salama.

Bw. Saleh alipofanya ukaguzi wa tiketi mtandao hivi karibuni alisema kuwa mwamko wa abiria kwenye matumizi ya mfumo wa tiketi mtandao kwa Mkoa wa Mbeya ni mkubwa na kwa magari yanayokaguliwa abiria ambaye hana tiketi ya mashine ya kielektroni basi anayo ile ya kwenye simu jambo ambalo linaonesha kuwa elimu ya matumizi ya mfumo huo imewafikia wadau.

"Sisi kama Mamlaka pamoja na Jeshi la Polisi na wadau wengine tutaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya mfumo huu ili kila mmoja wetu aelewe faida zake," ameeleza Bw. Saleh

Akielezea faida za mfumo huo, Bw. Saleh amesema mfumo wa Tiketi Mtandao unamwezesha abiria kukata tiketi kutokea mahali popote na kuepukana na adha za wapiga debe na kwa upande

*Inaendelea uk wa 6*



# MBEYA NA RUKWA WAPATIWA ELIMU YA TIKETI MTANDAO

*Inatoka uk wa 5*

wa wasafirishaji wanaweza kudhibiti mauzo ya tiketi kwa kuwa mfumo unawawezesha kuona mauzo yote yanayofanyika kupitia simu za mkononi na vilevile Serikali inapata mapato yake na hivyo amewasihi wananchi kuendelea kujifunza na kutumia tiketi mtandao

Naye Bw. Nyiga alisema, “tiketi hizi za mtandao zinamwezesha abiria kuchagua kiti anachokitaka na basi analolitaka ambapo kwa zamani suala kama hili lilikuwa na changamoto na abiria walikuwa wanagombaniwa lakini kwa sasa abiria akishakata tiketi yake anaelekea moja kwa moja kwenye gari alilokata na kukaa kwenye kiti alichokichagua na kusafiri kwa amani. Kwakweli mfumo huu unawaondolea bugudha wananchi’”, alifafanua

Kwa upande wake SP Gumha amewasihi wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga Mkoani Rukwa kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao ili kuepukana na usumbufu kwakuwa wanaweza kukata tiketi hizo sehemu yoyote na wakati wowote

Vilevile amesema, LATRA na Jeshi la Polisi wataendelea kushirikiana ili kuhakikisha kwamba wananchi wote na




wasafirishaji wanapata uelewa wa matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao kwa kuwa mfumo huo una faida kubwa kwa wananchi, mmiliki na Serikali kwa jumla.

Akizungumzia matumizi ya tiketi hizo Bi. Prisca Ngoli ambaye ni abiria alipongeza LATRA kwa kutengeneza mfumo rafiki ambao umesaidia kuondoa usumbufu uliokuwepo awali wa kutumia gharama za usafiri kwenda kukata tiketi kwenye vituo vya mabasi.

“Kwa kweli mfumo huu ni mkombozi sana kwetu nakumbuka tulipokuwa tunatumia ule mfumo wa zamani tulikuwa tunakatiwa tiketi moja watu wawili yaani tukiingia kwenye basi ni vurugu maana kila mmoja anataka kukaa kwenye kiti alichokata tiketi lakini kwa mfumo huu wa sasa purukushani hizo hakuna, abiria unakata tiketi kwenye simu yako na ukija unakuta kiti chako kiko wazi,” alieleza Bi. Prisca

Kwa upande wake Bw. Abbas Mwambenja amesema kuwa mfumo wa Tiketi Mtandao umesaidia kutozwa nauli halali zilizotolewa na kuidhinishwa na LATRA tofauti na mfumo wa zamani ambapo wananchi walikuwa wanatozwa nauli kiholela.

“Mimi ninafurahia sana mfumo huu, Wakala kanikatia tiketi nikapata ujumbe mfupi kwenye simu yangu na haikuchukua muda mrefu nikapatiwa risiti ya kwenye mashine na hii inasaidia maana hata tiketi ikipotea, nitaonesha hii ya kwenye simu yangu, kwa kweli huduma hii nimeipenda sana” amefafanua Bw. Mwambenja

Naye Bw. Uswege Mwandambo, dereva wa basi la Kampuni ya New Force linalotoka Mbeya kwenda Dar es Salaam alisema kuwa kwa sasa abiria wengi wamekuwa na uelewa mkubwa wa kutumia tiketi mtandao tofauti na siku za mwanzoni mfumo ulipoanza kutumika.

# BANTU: CHUKUENI TAHADHARI MNAPOPITA KWENYE MIUNDOMBINU YA RELI

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Bw. Henry Mgalla Bantu amewataka wananchi kuendelea kulinda miundombinu ya reli na kuchukua tahadhari pindi wanapokuwa karibu na miundombinu ya hiyo.

Bw. Bantu amesema hayo Oktoba 10, 2022 katika hafla ya ufunguzi wa wiki ya usalama wa reli nchini iliyofanyika Dar es Salaam katika Viwanja vya Ofisi ya Reli- SGR.

Aidha, Bw. Bantu amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuimarisha miundombinu ya reli pamoja na kuboresha huduma zake hivyo wananchi nao wanatakiwa kuhakikisha kuwa jitihada za serikali haziendi bure kwa kuwa mstari wa mbele kuilinda miundombinu hiyo.

Ameongeza kuwa, ili kuhakikisha usalama wa miundombinu ya reli na watumiaji, ni lazima kuwepo na mikakati madhubuti ya kuhakikisha jamii inapata elimu ya usalama wa reli, "Niwapongeze Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, LATRA, Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) kwa hatua madhubuti wanazochukua kuendelea kuhakikisha jamii zinakuwa salama kutokana na shughuli za usafiri wa reli. Endeleeni na jitihada hizi za kutoa elimu na kuhakikisha jamii na miundombinu ya reli inakuwa salama,"ameeleza Bw. Bantu



*Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Bw. Henry Mgalla Bantu akizungumza wakati wa ufunguzi wa wiki ya usalama wa reli nchini iliyofanyika Dar es Salaam katika Viwanja vya Ofisi ya Reli- SGR.*

Vilevile amesema kuwa, elimu hiyo itolewe mpaka vijijini ili kufikia watanzania walio wengi na ni vema kuwashirikisha na viongozi wa Serikali katika maeneo hayo ili kuweza kuwaeleza wananchi kuhusu usalama wa reli na usalama wao wanapopita kwenye maeneo ya reli.

Pia amesema, kazi kubwa inatakiwa kufanyika katika kubadili mitazamo ya watu kuhusu masuala ya reli kwa kuwa usalama wa reli ni wa kila mtanzania, "SGR itakapoanza hapa, treni zitakuwa zinaenda kwa mwendo kasi hivyo tusipozingatia suala la usalama tunaweza kupoteza maisha, kwahiyo usalama katika reli si jambo la kupuuza", amefafanua Bw. Bantu

Naye Mkurugenzi Mkuu TRC Bw. Masanja Kadogosa amesema kuwa usalama wa reli ni jambo linalopewa kipaumbele katika uwezeshaji wa usafiri wa reli duniani kote na TRC wamekuwa wakifuata taratibu na kanuni za usalama zilizowekwa kwa taasisi za Kimataifa na za Kikanda kwa maana ya Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Sheria za hapa nchini ikiwemo Sheria ya Reli Na. 10, 2017 na

***Inaendelea uk wa 8***

# BANTU: CHUKUENI TAHADHARI MNAPOPITA....



*Inatoka uk wa 7*

kanuni zake

"Kitu cha kwanza kabisa katika reli ni usalama, tukizungumzia SGR, kosa dogo linaweza kuleta madhara makubwa kwahiyo ni lazima tuweze kubadili mitazamo yetu kuhusu uendeshaji wa treni hizo ili kupunguza makosa ya kibinaadam yanayoweza kutokea. Tunakoelekea, tutakuwa tunaisikiliza sana LATRA kwa miongozo mtakayotupatia kwa kuwa ndio mdhibiti wa usafiri ardhini ikiwemo usafiri wa reli,"amefafanua Bw. Kadogosa.

Wiki ya reli inaadhimishwa Oktoba kila mwaka kwa nchi wanachama wa SADC kupitia Shirikisho la Reli Kusini mwa Afrika (SARA) na Kaulimbiu ya maadhimishi hayo ni Chukua Tahadhari, Treni Zina Mwendo wa Haraka, ni Hatari na inafanyika kuanzia Oktoba 10 hadi 16, 2022.

# MADEREVA WATAKIWA KUFUATA SHERIA, KUTOBUGHUDHI ABIRIA



Viongozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wamewataka madereva wa mabasi ya masafa marefu kufuata Sheria ili kuepusha ajali katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa mwaka.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara (LATRA) Bw. Johansen Kahatano na Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani SACP Ramadhani Ng'anzi Novemba 23, 2022 walipokutana katika Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam na kujadili namna bora ya kudhibiti mwendokasi wa mabasi ya masafa marefu kuelekea msimu wa mwisho wa mwaka.

Aidha, Bw. Kahatano aliwaasa wadau wa sekta ya usafiri ardhini nchini hasa wasafirishaji, madereva, makondakta na mawakala wanaokata tiketi kuzingatia Sheria na kuitii bila shuruti, "sisi hatutakuwa na muhali na mtu yeyote na atakayekiuka Sheria atakumbana na mkono wa Sheria, kwahiyo nawasihi kuwa kila mdau atimize wajibu wake."

Naye Kamanda wa Jeshi la Polisi Kikosi ca Usalama Barabarani SACP Ramadhani Ng'anzi alisema kuwa Jeshi hilo limejipanga vizuri kuhakikisha kwamba wale wanaokiuka sheria za usalama barabarani wanachukuliwa hatua bila kuoneana aibu, "Tuna imani kuwa madereva ambao wana leseni na wamepitia katika vyuo vya mafunzo ya udereva watafuata kanuni zinazowaongoza barabarani, sisi kama Jeshi la Polisi hatutosita kuchukua hatua stahiki kwa

*Inaendelea uk wa 9*

## MADEREVA WATAKIWA KUFUATA SHERIA, KUTOBUGHUDHI ABIRIA

*Inatoka uk wa 8*

yeyote atakayebainika anavunja Sheria ya Usalama Barabarani."

"Tunashukuru wenzetu wa LATRA wameanzisha mfumo wa tiketi mtandao ambao umesaidia sana kudhibiti wale wanaozidisha nauli kiholela na hivyo nawasihi wale wanaokata tiketi wazikate kwa njia ya mtandao. Kwa madereva nawasihi wafuate kanuni na alama zinazowaelekeza barabarani vinginevyo wasije wakatulaumu," alisisitiza SACP Ng'anzi.

LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabara wanafanya kazi kwa ukaribu kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti katika sekta ya usafiri ardhini na hasa katika kuhakikisha kuwa suala la ajali linapungua nchini

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI
Omba Leseni ya LATRA
Popote Ulipo
Kupitia: rrims.latra.go.tz
LATRA
www.latra.go.tz
LAND TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY

# KANALI MAIGA: ZINGATIENI MATUMIZI YA TIKETI MTANDAO




*Mkuu wa Wilaya ya Rombo Mhe. Kanali Hamis Maiga akizungumza na wananchi pamoja na vyombo vya habari wakati wa ukaguzi wa pamoja wa mabasi ya masafa marefu uliofanywa na LATRA*

Mkuu wa Wilaya ya Rombo Mhe. Kanali Hamis Maiga amewataka wasafirishaji kuzingatia matumizi ya Tiketi Mtandao na amewasihi abiria kuhakikisha wanapatiwa tiketi hizo pindi wanaposafiri.

Kanali Maiga alisema hayo Desemba 7, 2022 alipomuwakilisha Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu wakati wa ukaguzi wa pamoja wa mabasi ya masafa marefu uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Jeshi la Polisi pamoja na wadau wengine wa usafirishaji katika Stendi Kuu ya Mabasi ya Manispaa ya Moshi Mkoani Kilimanjaro

Akizungumzia faida za mfumo huo, Kanali Maiga alisema "mfumo huu una manufaa mengi, ukiachana na kuipatia Serikali mapato, unamuondolea abiria bugudha kama vile kuzidishiwa nauli kwa baadhi ya wasafirishaji ambao sio waaminifu katika kazi zao na pia unamsaidia mmiliki wa gari kupata stahiki zake kwakuwa anaona na kupata mapato yake papo hapo baada ya abiria kukata tiketi,"ameeleza Kanali Maiga.

Naye Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Kilimanjaro Bw. Paul Nyello alisema kuwa Serikali imeelekeza kutumika kwa tiketi za kielektroni kwahiyo kila msafirishaji anatakiwa kufuata maelekezo hayo "sisi kama LATRA tunajitahidi kutoa elimu kuhusu utekelezaji wa matumizi ya mfumo huu laki-

*Inaendelea uk wa 10*



# KANALI MAIGA: ZINGATIENI MATUMIZI YA TIKETI MTANDAO

*Inatoka uk wa 9*

ni endapo itatokea ukiukwaji wa Sheria, hatutosita kuwachukulia hatua,"alisema Bw. Nyello

Naye Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabari Mkoa wa Kilimanjaro SSP Pili Misungwi amewataka abiria kuhakikisha kuwa taarifa zao muhimu zinakuwepo kwenyemfumo waTiketi Mtandao ikiwa ni pamoja na jina, sehemu anapotoka, anapokwenda, muda wa basi kuondoka, kiti alichochagua, nauli iliyokatwa na kadhalika na amewasihi kukagua taarifa hizo ili kujiridhisha kabla ya kuanza safari na pindi wanapobaini kuwa taarifa zilizopo sio sahihi watoe taarifa LATRA au Jeshi la Polisi ili kupata msaada wa haraka.

Vilevile amewataka wasafirishaji kutoa tiketi mtandao kwa abiria, "ninawasihi watoa huduma kufuata agizo la Serikali la kutumia tiketi mtandao ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza maana sisi Jeshi la Polisi tunasimamia Sheria na suala la tiketi mtandao lipo kisheria hivyo kwa msafirishaji atakayekiuka agizo hili atakuwa anakiuka Sheria na hivyo




tutamchukulia hatua kulingana na Sheria," alisisitiza

Bw. Innocent Kimbisa ambaye ni abiria alisema, "naufurahia sana mfumo wa tiketi mtandao kwasababu kwa sasa sisumbuliwi na yeyote, ninachokifanya ni kuingia kwenye mfumo kupitia simu yangu, ninachagua basi ninalolitaka kwa ajili ya safari yangu, ninalipia na ninaenda moja kwa moja kwenye basi naonesha ujumbe ambao ndio tiketi yangu kasha nakaa kwenye kiti nilichochagua bila changamoto yoyote na tena siku hizi hakuna kugombania kiti kama ilivyokuwa zamani,"alisema.

Naye dereva wa basi Bw. Zuberi Athanas alisema kwa mfumo wa tiketi mtandao, kwasasa abiria wana uhakika na safari zao na nauli wanazolipia kwakuwa ndani mfumo zimewekwa nauli elekezi zinazotolewa na kuidhinishwa na LATRA.

Kwa upande wake, Afisa Msimamizi wa Kodi TRA Mkoa wa Kilimanjaro Bw. Odupoi Papaa alisema kuwa mfumo wa tiketi mtandao unasaidia Serikali kupata mapato yake ambayo yanaenda kutekeleza masuala mengine ya maendeleo kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara kwahiyo mwananchi anauhakika kuwa kiwango kilichokatwa kimeifikia Serikali moja kwa moja tofauti na hapo awali.

tiketi MTANDAO

# LATRA YAPONGEZWA KWA KUANDAA MKUTANO NA WADAU WA TEKSI MTANDAO



*Mkuu wa Wilaya Ilala Mhe. Ng'wilabuzu Ludigija (katikati) akiwa na wadau waliohudhuria mkutano wa Teksi mtandao. Kulia Kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo na kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Mkutano huo Bw. Ahmed S. Kilima*

Mkuu wa Wilaya Ilala Mhe. Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kutekeleza dhana ya ushirikishaji kama moja ya msingi wa utawala bora kwa kuandaa mkutano wa wadau wenye lengo la kupokea maoni kuhusu marejeo ya viwango vya nauli ya teksi mtandao

Mhe. Ludigija amesema hayo Oktoba 11, katika ukumbi wa Arnatoglou alipofungua Mkutano wa Wadau kuhusu marejeo ya viwango vya nauli za Teksi Mtandao nchini kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla

Aidha, Mhe. Ludigija amesema "moja ya misingi ya utawala bora ni ushirikishwaji, nasi kama wadau kwa upande wa Serikali tumefurahi kushuhudia ushiriki wenu wadau katika Mkutano huu muhimu wa kutoa maoni yenu ili kuipa LATRA taarifa zitakazoisaidia kufanya maamuzi."

Ameongeza kuwa, Usafiri wa magari ya kukodi ni muhimu katika kuongeza wigo wa huduma za usafiri kwa abiria hususan mijini, ili kuwezesha shughuli za kiuchumi kufanyika kwa wakati na kuboresha maisha ya Watanzania.

Vilevile amewapongeza wabunifu na wawekezaji wote ambao wametengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayowezesha kusimamia huduma za usafiri wa teksi mtandao lakini pia ameitaka LATRA kuongeza usimamizi wa utendaji wa mifumo hiyo kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo, kwa kujali maslahi mapana ya watumia huduma, wawekezaji na wananchi wote kwa jumla.

"Kwa kuwa jukumu tunalofanya leo ni kupokea mapendekezo, kuyajadili na kutoa maoni, nawasihi kila mmoja wetu, kwa kuzingatia wajibu wake, kutoa maoni yake kwa uhuru na kwa lugha yenye staha. Natoa rai kwenu wadau kuitumia vizuri nafasi hii, ili kuwawezesha wataalamu wetu kufanya kazi yao kwa ufanisi", ameeleza Mhe. Ludigija.

Naye Mkurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Suluo amesema Kwa mujibu wa Kifungu cha 19 (3) cha Sheria Sura 413, baada ya kuzingatia maoni ya wadau, Mamlaka ilitangaza Nauli Elekezi za teksi mtandao kwa Tangazo Na. LATRA/01/2022 la tarehe 14/3/2022 ambalo lilitolewa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 8/4/2022 kwa Tangazo Na. 1369 ambalo liliainisha viwango vya nauli ya teksi mtandao.

Aidha, amesema kuwa, wakati wa utekelezaji wa nauli za teksi mtandao, Mamlaka kwa nyakati tofauti, ilipokea malalamiko kutoka kwa wadau hawa (Bolt na Uber) lakini pia kutoka kwa madereva wa teksi mtandao kupitia chama chao – Tanzania Online Drivers Association (TODA) na hivyo Mkutano huo umeandaliwa

***Inaendelea uk wa 12***

## LATRA YAPONGEZWA KWA KUANDAA MKUTANO NA...

*Inatoka uk wa 11*

ili kupokea maoni kuhusu viwango vya nauli vilivyopo kwa lengo la kutatua changamoto zao kuhusiana na viwango hivyo.

CPA Suluo ameongeza kuwa, baada ya kukamilisha zoezi la kupokea maoni ya wadau, Menejimenti ya LATRA itafanya tathmini na kuwasilisha mapendekezo kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA kwa uamuzi na mapendekezo ambayo yatawasilishwa kwa Mamlaka za Serikali (Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali). Baada ya idhini ya Mamlaka za Serikali, nauli zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali, na zitaanza kutumika siku 14 baada ya kutangazwa kwa mujibu wa Kanuni.

Mkutano huo ulioandaliwa na LATRA, umefanyika katika ukumbi wa Arnatoglou uliopo mnazi mmoja Dar es Salaam, umehusisha wadau mbalimbali kama vile Makampuni ya Teksi Mtandao (Bolt, Uber,Little Ride, Paisha, InDrive, nk), Madereva wa Teksi Mtandao, Wamiliki wa Magari ya Teksi Mtandao, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC) na wadau wengine.

## MADEREVA MBEYA NA RUKWA WAPEWA ELIMU YA UTHIBITISHAJI WA MADEREVA



*Afisa Mfawidhi Mkoa wa Rukwa Bw. Athumani Nyiga akiwapa elimu ya usajili na uthibitishaji wa madereva kwa madereva wa magari ya mizigo Manispaa ya Sumbawanga, Rukwa.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kupitia Afisa Mfawidhi Mkoa wa Rukwa Bw. Athumani Nyiga pamoja na Afisa Mfawidhi Mkoa wa Mbeya Bw. Omary Saleh imetoa elimu ya Uthibitishaji wa Madereva kwa madereva wa vyombo vya usafiri kibiashara katika mikoa hiyo kwa lengo la kuwafahamisha umuhimu wa kuthibitishwa na LATRA kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya LATRA Sura ya 413.

Akizungumza na madereva kuhusu umuhimu wa kuthibitishwa na LATRA, Bw. Saleh amewaambia kuwa uthibitishaji unayofanywa na Mamlaka itaifanya tasnia ya udereva hapa nchini kuheshimika na kutambulika kama zilivyo kazi nyingine na hivyo kuongeza thamani ya dereva mmoja mmoja hapa nchini, vilevile dereva huyo anaposajiliwa na kuthibitishwa atakuwa na wigo mpana wa kufanya kazi kwenye nchi za Afrika kwa kuwa atatambulika kwenye nchi wanachama za EAC, COMESA na SADC.

"Nadhani wote tunajua mtu ukisimama na kusema mimi ni dereva picha zinazojengeka vichwani mwa watu, ni tofauti na mtu akisimama na kusema mimi ni rubani au hata mimi ni nahodha wa meli. Sasa tutakapokuthibitisha wewe kama dereva unaenda kuheshimika katika kazi yako,"alisema Bw. Saleh.

Naye Afisa Mfawidhi Mkoa wa Rukwa Bw. Athumani Nyiga aliwaambia madereva hao kuwa suala laUthibitishaji ni la Kisheria na hivyo amewasihi madereva hao kujisajili kwa kutumia namba yake ya NIDA kwenye mfumo

*Inaendelea uk wa 13*



# MADEREVA MBEYA NA RUKWA WAPEWA ELIMU YA UTHIBITISHAJI WA MADEREVA



***Moja ya Madereva waliojitokeza kwaajili ya kufanya mtihani ili kuthibitishwa***

***Inatoka uk wa 12***

mama wa RRIMS kupitia anuani ya https://rrims.latra.go.tz/ login na kuweka nafasi ya kufanya mtihani (booking) na kisha kuchagua tarehe na muda atakaopenda kufanya mtihani.

Naye Bw. Pascal Mwantosya, mara baada ya kupatiwa elimu hiyo alisema,"Elimu mliyotupatia leo ni muhimu sana na sisi madereva tukithibitishwa hakika sekta yetu ya udereva itakuwa katika hali nzuri na ya heshima. Pia kupitia kuthibitishwa naona madereva tutakuwa makini tunapokuwa kwenye majukumu yetu na hii itasaidia kupunguza ajali kwa kiasi kikubwa. Mimi nipo tayari kuthibitishwa."

Kwa upande wake Bw. David Ndunguru dereva wa magari makubwa ya mizigo amewahimiza madereva wengine kujitokeza kwa lengo la kusajiliwa na kuthibitishwa na LATRA kwa kuwa ni jambo lenye manufaa zaidi kwao.

"Kutokana na elimu tuliyopewa nimegundua kuwa dereva akishathibitishwa anakuwa ametambulika rasmi na anaweza kufanya kazi popote ndani na nje ya nchi. Hivyo ninawashauri madereva wengine tuungane kwa pamoja ili tudhibitishwe" alionge-za Bw. Ndunguru.

Suala la uthibitishaji wa madereva lipo kisheria ambapo kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (i)(e) cha Sheria ya LATRA Sura ya 413, LATRA imepewa jukumu la kuwasajili na kuwathibitisha Madereva na Wahudumu wa Vyombo vya Usafiri Kibiashara. Hadi kufikia Novemba 2022, zaidi ya madereva 700 wameshafanya mtihani kwa lengo la kuthibitishwa.



# CPA SULUO: TUNAWEZA KUACHANA NA NISHATI HATARISHI KWA MAZINGIRA

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) CPA Habibu Suluo amesema ni muhimu nchi za Afrika kufikiria matumizi ya nishati rafiki kwa mazingira katika shughuli za usafirishaji ikiwemo usafiri wa reli.

CPA Suluo ameyasema hayo Desemba 2, 2022 wakati akifunga rasmi mafunzo ya siku tano kwa wataalamu zaidi ya 40 wa usafiri wa reli kutoka nchi 15 za Afrika yaliyofanyika Chuo cha Utumishi wa Umma - Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo yaliandaliwa kwa ushirikiano wa LATRA na Chuo Kikuu cha Birmingham cha nchini Uingereza.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) CPA Habibu Suluo akifunga rasmi mafunzo ya siku tano kwa wataalamu zaidi ya 40 wa usafiri wa reli kutoka nchi 15 za Afrika yaliyofanyika Chuo cha Utumishi wa Umma - Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao jijini Dar es Salaam.*

"Ukiangalia sehemu kubwa sana ya matumizi ya reli 'Diesel' inatumika, kwa wenzetu mfano Uingereza wana mpango kuwa ifikapo mwaka 2040 wawe wameachana kabisa na matumizi ya 'Diesel.' Hivyo kupitia mafunzo haya tumepata kufahamu kuwa inawezekana kabisa kuachana na nishati ambayo si rafiki kwa mazingira katika usafiri wa reli hivyo nchi za Afrika zinatakiwa kujipanga vizuri kwani usafiri wa reli unaziunganisha nchi nyingi za Afrika" amesema CPA Suluo.

Akiyazungumzia mafunzo hayo Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli kutoka LATRA Mhandisi Hanya Mbawala kama mmoja wa waliopata mafunzo hayo amesema kuwa mafunzo yameongeza uwanda wa kufikiria nishati mbadala itakayotumika katika uendeshaji wa treni.

"Tumeangalia kuna umuhimu wa kutoka kwenye nishati ya 'Diesel' na Umeme ambayo ndio inatumika kwa sasa na kuhamia kwenye nishati mbadala ya 'Hydrogen' ambayo itakuwa rafiki zaidi na kufanya usafiri wa reli kuwa bora na salama. Hii ni nishati mpya kabisa na maandalizi yake yameshaanza na sisi Tanzania tumechaguliwa kuwa sehemu ya majaribio ya nishati hii" amesema Mhandisi Mbawala.

Akizungumzia faida alizozipata kutoka kwenye mafunzo haya Bw. Joseph Michael Afisa Mfawidhi wa LATRA mkoa wa Manyara, amesema kuwa mafunzo hayo yamekuwa fursa ili kuendana na nishati ambayo ni rafiki kwa mazingira.

"Tumejengewa maarifa makubwa ya njia ambazo tutatumia nishati rafiki kwa mazingira, mfano matumizi ya nishati ya 'hydrogen' na umeme ambao kwa kiasi kikubwa hauchafui mazingira. Pamoja na hayo tumeweza kujadili mikakati ambayo tutaitumia ili kushawishi serikali zetu kuanza kutumia nishati mbadala ambayo ni salama na rafiki kwa mazingira" amesema Bw. Michael.

Mafunzo hayo yamekuja wakati dunia ikikabiliana na janga la mabadiliko ya tabia nchi ambayo kwa kiasi kikubwa yametokana na shughuli za kibinadamu ikiwemo usafirishaji ambapo vyombo vya usafiri vitumiavyo nishati ya mafuta hutoa hewa ya ukaa ambayo huchangia kuathiri tabaka la 'Ozon'.

# MADEREVA WATAKIWA KUSHIRIKIANA NA LATRA, JESHI LA POLISI




*Mkuu wa Wilaya ya Rombo Mhe. Kanali Hamis Maiga akizungumza na madereva wakati wa ukaguzi wa pamoja wa mabasi ya masafa marefu uliofanywa na LATRA, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, na Jeshi la Polisi pamoja katika Stendi Kuu ya Mabasi ya manispaa ya Moshi*

Mkuu wa Wilaya ya Rombo Mhe. Kanali Hamis Maiga amewataka madereva wa mabasi ya masafa marefu Mkoa wa Kilimanjaro kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani katika majukumu yao na pia amewataka kuzingatia Sheria na Kanuni za Usalama Barabarabi ili kuepuka ajali zinazogharimu maisha ya wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu wakati wa ukaguzi wa pamoja wa mabasi ya masafa marefu uliofanywa na LATRA, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Jeshi la Polisi pamoja na wadau wengine wa usafirishaji katika Stendi Kuu ya Mabasi ya manispaa ya Moshi Mkoani Kilimanjaro, Kanali Maiga alisema madereva wakiwa karibu na LATRA na Jeshi la Polisi, itakuwa rahisi katika kutekeleza Sheria za Usalama Barabarani.

Kanali Maiga aliongeza kuwa, ni wajibu wa madereva kuzingatia mwendo ulioidhinishwa na Serikali ili kupunguza na kuondokana na tatizo la ajali ambazo zimekuwa zikiondoa nguvu kazi ya Taifa.

"Suala la ajali kipindi cha mwisho wa mwaka katika Mkoa huu wa Kilimanjaro limekuwa ni tatizo kubwa na tumekuwa tukipoteza wananchi ambao ndio chachu ya kuleta maendeleo katika mkoa wetu na Taifa kwa jumla, hivyo nawasihi madereva kuacha kuendesha mabasi kwa mwendokasi ili kuyalinda maisha ya wananchi kwa mustakabali mzuri wa maisha yao na familia zao," Kanali Maiga alieleza

Naye Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Kilimanjaro Bw. Paul Nyello alizungumzia mabasi ya hakuna kulala ambayo yamekuwa yakifanya biashara ya usafirishaji usiku na alisema kuwa LATRA inatoa onyo na inawakumbusha kutekeleza majukumu yao kulingana na leseni walizonazo na vinginevyo Mamlaka itachukua hatua kwa kuwa wanachofanya ni kinyume na taratibu zilizopo.

"Tunawaasa abiria ambao wamekuwa wakipanda mabasi hayo waache hiyo tabia kwakuwa wanahatarisha maisha yao maana wale madereva hawapumziki wanafika mwisho wa safari na wanageuza jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao, tujaribu

***Inaendelea uk wa 16***



## MADEREVA WATAKIWA KUSHIRIKIANA NA LATRA, JESHI LA POLISI

*Inatoka uk wa 15*

kuyajali maisha yetu kwanza kabla ya kufikia hatua ya kupanda kwenye hakuna kulala. Watumie vyombo sahihi vilivyothibitishwa na LATRA kwa ajili ya usalama wao na familia zao,"

Akizungumzia suala la mwendokasi, Bw. Nyello alisema, LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wamejipanga kuhakikisha kuwa madereva wanaendelea kupata elimu ya usalama barabarani lakini pia ikitokea wanaenda kinyume na Sheria na taratibu zilizopo hawatasita kuchukua hatua kali dhidi yao.

Akizungumzia kipindi cha mwisho wa mwaka, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro ACP Simon Maigwa alisema Mkoa huo upo salama na wanaendelea kudhibiti matukio ya ajali na hiyo ni kutokana na mipango thabiti waliyonayo kwa kushirikiana na LATRA pamoja na vyombo vingine vya usalama hapa nchini

"Natoa rai kwa yeyote anayeingia mkoa wa Kilimanjaro anazingatia Sheria za usalama barabarani. Tutaendelea kufanya ukaguzi wa mabasi tukishirikiana na LATRA ili kuhakikisha kuwa masuala haya ya usalama yanazingatiwa na kufuatwa na madereva wetu ili kuepukana na ajali," ACP Maigwa alisisitiza.

## MHE. LUDIGIJA AFUNGUA MKUTANO WA WADAU WA TEKSIMITA



Mkuu wa Wilaya Ilala Mhe. Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija amesema Serikali ya awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya juhudi za kipekee kuhakikisha inakuza sekta binafsi kwa kuhakikisha sekta hiyo inakuwa chachu ya kusukuma uchumi na chanzo cha mapato ya serikali kupitia kodi na kuongeza ajira kwa vijana hasa kwenye huduma za usafiri ardhini ikihusisha magari ya kukodi na huduma za usafiri wa mijini kwa kutumia mabasi na pikipiki za miguu miwili na mitatu.

Mhe Ludigija amesema hayo Desemba 14, 2022 katika Ukumbi wa Mkutano Karimjee jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa wadau wa kupokea maoni ya kuhusu utaratibu wa matumizi ya mita za teksi (taximeter) kwenye usafiri wa teksi za kawaida ambazo hutumika kwa kukodishwa kwa safari binafsi hapa nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam Mhe. Amos Makala, Mhe. Ludigija amesema kuimarika kwa miundombinu ya barabara katika maeneo mengi hapa nchini imesaidia kuimarika kwa usalama na ubora wa huduma za usafiri wa barabara na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji uchumi.

Akizungumzia teksimita,

*Inaendelea uk wa 17*

# MHE. LUDIGIJA AFUNGUA MKUTANO WA WADAU WA TEKSIMITA




*Mfano wa Teksimita ambazo zinatumiwa katika nchi mbalimbali*

*Inatoka uk wa 16*

Mhe. Ludigija alisema kuwa matumizi ya teksimita yatasaidia kukokotoa kiwango cha nauli atakachotakiwa kulipa mteja baaada ya kufika mwisho wa safari na hivyo aliwasihi wadau wote waliohudhuria kikao hicho kutumia fursa ya kutoa maoni ili kuwezesha upatikanaji wa mawazo chanya yatakayosaidia kupata utaratibu mzuri wa uendeshaji wa teksimita ili kila mmoja anufaike nazo," alieleza

"Niwapongeze sana LATRA katika hili kwasababu wamekuwa wakishirikisha wadau kabla ya kufanya uamuzi kwenye masuala mbalimbali na hivyo nizisihi taasisi nyingine kuiga jambo hili jema linalofanywa na LATRA," alisisitiza

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu LATRA, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA Bw. Johansen Kahatano alisema "Jukumu hili la ushirikishaji umma ni zao la utawala bora ambapo inasisitizwa kushirikisha wadau kwenye utekelezaji wa majukumu ya kiudhibiti ambayo misingi yake imejengwa kwenye Sheria ya LATRA ya mwaka 2019 na kanuni zake."

Vilevile Bw. Kahatano aliongeza kuwa kwa kutambua si kila mdau anaweza kufika katika mkutano huo, Mamlaka imeweka utaratibu wezeshi wa kuendelea kupokea maoni kwa njia ya maandishi hadi tarehe 31 mwezi Desemba mwaka huu ambapo mdau anaweza kuwasilishwa kwa kuyafikisha katika ofisi za Mamlaka zilizopo mikoa yote au kwa barua pepe ya dg@latra.go.tz.

Aidha alifafanua kuwa, kwa mujibu wa kanuni ya 15 (d)ya Kanuni za LATRA za Vyombo vya Kukodi za mwaka 2020, vyombo vyote vinavyopewa leseni ya usafiri wa kukodi vinatakiwa kuwa na mita ya nauli au mfumo unaweza kukukotoa nauli.

Jarida hili limeandaliwa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kikiongozwa na Bodi ya Wahariri


**MWENYEKITI**
CPA Habibu Suluo

**MHARIRI MKUU**
Samuel Keenja

**WAHARIRI WASAIDIZI**
Salum Pazzy
Abdallah Mhagama

**MWANDISHI**
Mambwana Jumbe

**MSANIFU PICHA**
Ibrahim Said

**MPIGA PICHA**
Deusdedity Masemba

**MSANIFU JARIDA**
Deusdedity Masemba


©2022